



# Tafsiri ya Kiswahili

Kitabu hiki kinapendekezwa kwa watoto wa umri wa miaka 10-14
*Mwandishi*: Hanneke van ‘t Veen, Uholanzi
*Muundo wa ukurasa wa nje*: Hanneke van ‘t Veen
*Michoro*: Hanneke van ’t Veen
*Tafsiri*: Vincent Gerald Vyamana

Shukrani za pekee ziwaendee Vincent Gerald Vyamana, Mary Ann George, Mirjam van ‘t Veen, Dabwiso Sakala, Douglas Spencer na Arlette van den Berg kwa maoni yao na msaada waliotoa, na kwa Maria Santos kwa kusimamia masomo ya Shahada ya Uzamivu ya Hanneke ambayo ndiyo msingi wa kitabu hiki.

**Hakuna haki zilizohifadhiwa.** Kitabu hiki kinaweza kuzalishwa, kutunzwa katika mifumo ya kuzalisha vitabu, au kusambazwa katika namna au njia yoyote, kielektroniki, mitambo ya kimakanika, nakala, rekodi, au njia nyinginezo zozote, bila kulazimika kuomba kwanza kibali cha maandishi toka kwa mwandishi. Hata hivyo mwandishi hatoi ruhusa ya nakili ya moja kwa moja ya sehemu yoyote ya kitabu inayokiuka kanuni za kiuandishi au kitaaluma zilizowekwa.

*“Kuufanya ulimwengu uwe bora kwa watu wote waishio ndani yake kupo mikononi mwako”*

~ Nelson Mandela ~



## Tedi ana ndoto

Kipindi kifupi kilichopita, katika nchi ambayo haiko mbali sana, msichana mwenye ndoto zake alijinyoosha akitawanya mikono yake. "Aah…", alipiga mwayo. "Ni siku nzuri kama nini kwa ajili ya kufanya ziara ya kusisimua!".
"Habari za asubuhi, Tedi!" wazazi wake walimsalimu kwa furaha. "Sisi tunakwenda kulima katika mashamba yetu."
"Mimi nakwenda maporini," Tedi alijibu. Akafunga nywele zake mabutu mawili makubwa yaliyoinuka juu ya kichwa chake. Mara akatembea kuelekea katika kingo za msitu. Huko, akapanda juu ya mti mrefu alioweza kuuona, akavuta pumzi kwa nguvu na kupiga kelele kwa uwezo wake wote, "HABARI ZA ASUBUHI TEMBO"
Kelele kubwa ya majani yaliyopukutika na matawi ya miti yaliyovunjika ikasikika. Mara tembo akaibuka kutoka vichakani, tembo mwenye miguu ya ajabu akamkimbilia Tedi kwa shauku. "TUUTUUTUUU!"
Tedi akatabasamu. Tembo akapunga mkonga wake hewani.
"Twende zetu!"

Kwa pamoja, Tembo na Tedi wakakimbia kukatiza katika msitu huku wakiangalia vipepeo, ndege tausi na matunda ya msituni yenye juisi. Tedi akaruka kwa wepesi toka juu ya mizizi ya miti hadi kimo cha usawa wa magoti ya tembo. Kando yake, Tembo akakatiza kwa kishindo katikati ya pori, vichaka na matawi ya miti, huku akiziba njia ya Tedi kupita. Walipochoka wote, wakajigalagaza na kulala chali wakiangalia bahari ya majani ya miti juu yao. Vazi la Tedi la rangi za blue na njano lilijaa madoa ya matope, na lilinasa majani na nyasi.

"Niliota ndoto ya ajabu, Tembo", Tedi akasema.
"Niliota kuwa nilikwenda shuleni na nikajifunza kusoma na kuandika. Nilisoma mamilioni ya vitabu kuhusu ndege na miti, na dunia tunayoishi. Mwishowe, nikajua kila kitu kuhusu mazingira asilia." Tedi akajigeuza kulalia ubavu wake. "Pia nimejua kila kitu kuhusu wewe Tembo pamoja na rafiki zako", Tedi akaongeza huku macho yake yaking'aa.
Tembo akaguna. Kana kwamba hutaweza kamwe kujua mambo yote kuhusu tembo maridadi kama mimi, ewe msichana mtukutu, alioneka kuwaza hivi.
Tedi akatabasamu. Akachuma jani na kulichunguza kwa makini, vidole vyake vikifuatisha migongo laini ya lile jani. Ghafra akashituka toka usingizini na kurudi katika hali halisi. Mabutu mawili ya nywele zake hayakuwepo tena kichwani mwake.
"Natamani kwenda shule katika maisha halisi pia," Tedi akasema kwa sauti ya upole. "Bahati mbaya, wazazi wangu hawana uwezo wa kunisomesha."
Tembo akamkazia macho yaliyong'aa mithili ya zabibu kavu zilizochomoza chini ya ngozi ya kijivu. Gahfla tembo akamkamata na kumwinua Tedi na akamzungusha kwa mkonga wake mpaka mabutu ya nywele zake yakarejea tena juu ya kichwa chake kama mwanzo.
"Upo sahihi, Tembo, siku moja nitakwenda shule!"
"TUUT!"



## Mgeni wa ajabu

Siku moja, Tedi alipokuwa anatoka nyumbani kwao, alinusa harufu ya mti ulionguzwa katika pua zake. Kwa udadisi, akageuka huku na huko na kuruka juu kwa mshangao. Akaona gunia la rangi ya kahawia likijongea kuelekea kwake. “Hujambo, msichana mpendwa,” gunia likasema.
Tedi akastaajabu. Hakujua kama abakie pale, akimbie au acheke. Mabutu ya nywele kichwani mwake yakatetemeka. “Jambo gani hili duniani hapa!” akawaza. “Najua watu hesema kuwa msitu huu ni wa miujiza, lakini gunia linaloongea? Hii ni mpya!”
Mara kichwa cha mtu kikachomoza juu ya gunia. Juu ya kichwa ilitulia kofia kubwa ya rangi ya damu ya mzee.
“JIna langu naitwa Jami, msichana mpendwa”, akasema mwanaume yule aliyeinua kichwa chenye kofia. “Unajua njia ya kwenda kijiji cha Mtakuja?” Tedi akatabasamu. Haraka, akakung’uta nguo yake akijaribu kuondoa majani na madoa yaliyokuwa yamenasa katika nguo hiyo wakati akipita msituni.
“Naitwa Tedi”, akajibu. “Ni sawa mzee, Mtakuja ni kijiji changu. Nifuate!”
Huku akitembea kwa hatua za haraka Tedi akamwongoza mtu yule mpaka Mtakuja, huku akiongea kwa shauku hukusu rafiki yake Tembo na ziara zao za msituni.

Wakati Tedi na Jami walipofika Mtakuja, paa za nyumba zilikuwa ziking’aa kwa rangi ya chungwa ya jua la jioni. Mbwa akabweka, Jami akaweka kofia yake vizuri kichwani na akamkazia macho kila mwanakijiji waliyekutana naye. “Ni mji uliochangamka kama nini, Tedi” Jami alisema. Je, inawezekana kuongea na kiongozi wa kijiji hiki kwa namna yoyote ile? Nina kitu muhimu cha kumwambia.”
Tedi akatikisa kichwa. “Hakuna shida, kiongozi wetu yupo hapa hapa!” Alisema na akanyosha mkono wake kwa mwenye hekima mmoja, ambaye macho yake huwatisha wanakijiji wote. Akiwa amezama katika mawazo, kiongozi wa kijiji alikuwa ameka juu ya stuli yake, alikuwa akiendelea kugongagonga penseli yake kwenye daftari ambalo alikuwa akiandika ndani yake.
“Huyu ni Jami, kiongozi wa kijiji,” Tedi akasema kwa kujigamba. “Ametokea mji mkubwa kuja kututembelea!”
Kiongozi wa kijiji cha Mtakuja akaangalia juu na kumtathimini Jami kuanzi ncha ya kofia yake hadi ncha ya vidole vya miguu yake. Ilioneka kana kwamba alitaka kujiridhisha kama ujio wa mgeni wa ghafla ungeongeza au kupunguza hofu zake.
“Karibu katika kijiji chetu, Jami,” hatimaye kiongozi wa kijiji alisema akionesha tabasamu la ukarimu. “Nikusaidie nini?”
“Kiongozi wa kijiji, nina fursa ambayo huwezi kuikataa!”, Jami aliongea kwa uchangamfu.
Jami akarusha gunia lake hewani, ambalo lilitapakaza harufu ya miti iliyochomwa kila mahali. “Ngoja nikueleze kuhusu dhahabu nyeusi niibebayo!”



## Dhahabu nyeusi

Wakiwa katika kudadisi juu ya uvumi wa dhahabu nyeusi, wanakijiji wa Mtakuja walijikusanya mmoja baada ya mwingine kwenye uwanja wa mikutano, uliokuwa umefunikwa na ulaini wa kusisimua kutokana na nyasi zilizoota juu ya mchanga. Jami akasimama katikati ya uwanja na kwa ukarimu akimsalimu kila aliyefika kwa kutumia ncha ya kofia yake kubwa ya rangi ya bluu. Wakati kila mmoja alipokuwa amekwishafika, akaingiza mkono wake ndani ya gunia lake kubwa taratibu na akatoa kitu mithili ya jiwe jeusi. "Tazama, dhahabu nyeusi", Jami akasema kwa uchangamfu.
Wanakijiji wakatazamana na wakaelekeza nyusi zao juu.
"Hiyo siyo dhahabu," akapiga kelele mmoja wa wanakijiji, aitwaye Mohamedi.
"Huo ni mkaa!"
"Mkaa?" Tedi alinong'ona.
"Mkaa ni chanzo cha nishati itokanayo na miti," Baba yake Tedi, Andrea, akajibu, huku akijikuna sharubu zake ndefu. "Watu waishio katika mji ule mkubwa hutumia mkaa kuwasha moto na kupikia chakula chao." Jami akatulia bila wasiwasi mpaka wanakijiji walipoacha kunung'unika.
"Wapendwa watu wa Mtakuja," alisema huku akipunga mkono hewani katika hali ya uchekeshaji.
"Sidhani kama mnatambua namna kipande cha mti hiki kidogo cheusi kilivyo na thamani! Maelfu, hapana, mamilioni ya watu katika ule mji mkubwa wanatumia mkaa kila siku. Uhitaji wa mkaa ni mkubwa sana na bei yake pia!"

Jami akatulia kwa mkao wa masihara. Wanakijiji wakabana pumzi. "Nichomeeni mkaa nanyi mtakuwa matajiri!". Jami akaukazia macho ule umati wa watu. Alifahamu fika matokeo makubwa ya hotuba yake kwa wanakijiji. Wanakijiji wakatazamana, macho yao yakitoa taswira ya mamilioni ya maneno yasiyotamkika.
"Loo," wazazi wa Tedi wakapaza sauti kwa pamoja. "Ni fursa ya ajabu kama nini. Tukipata hiyo hela tunaweza kumpeleka Tedi shule".
"Lazima itakuwa imani yako kwa Mungu ndiyo imesababisha ukutane na Jami katika msitu, Tedi," mama yake Tedi, aitwaye Lea alisema. Akapigapiga mabutu ya bintiye. "Hakika lazima ilikuwa hivyo," Tedi akajibu.
"Siwezi kuchelewa kumwambia Tembo!"
Akakimbia mara moja kuelekea msituni.
"TEMBO!"
"TUUTUUTUUT!"


MAKAA

## Jami atoa darasa kwa ubobezi

“Yeyote aahidiye dhahabu isiyo halisi hawezi kuaminiwa!” alisema Mohamedi. Alikuwa amepishanisha mikono yake. Wanakijiji wengi wakatikisa vichwa vyao.
“Nakubaliana kuwa kuita mkaa dhahabu nyeusi inaleta mashaka. Sitarajii kuwa inaweza kutufanya tuwe matajiri. Lakini inafaa tuijaribu!” akadakia mmoja wa marafiki wa Mohamedi. “Hapa ni sawa na kwamba hatuna kipato chochote. Chanzo chochote cha hela ya ziada kitapokelewa ili kitusaidie kununua chakula na kupeleka watoto wetu shule.” “Ndiyo”, wakakubali wanakijiji wengine waliosalia. “Yafaa tuijaribu hii!”
Ilipokuwa dhahiri kuwa wanakijiji walio wengi walikuwa na shauku ya kuchoma mkaa, kiongozi wa kijiji cha Mtakuja alisimama na kumpa mkono Jami.
“Tunakuamini Jami,” akasema. “Tunaipokea fursa. Tuna swali moja tu. Tunaweza kuchoma mkaa namna gani?”
Wanakijiji wote wakamgeukia Jami, aliyetabasamu kana kwamba alikuwa amekwisha badilisha mkaa kuwa dhahabu.
“Asante kwa kuniamini, kiongozi wa kijiji. Hutajuta, nakuahidi. Nifuateni msituni nitawaonesha namna ya kutengeneza mkaa!”

Kwa shauku kubwa Jami aliwatangulia wanakijiji wale kuelekea katika ukingo wa msitu ili kuwapa darasa kwa ubobezi kuhusu uchomaji mkaa. Wanakijiji wakamfuata, baadhi wakiwa na matumaini makubwa na wengine wakisitasita.
Hatua ya kwanza unakata miti, Jami akafafanua. “Miti michache tu”.
Akatoa mashoka mawili toka katika begi lake kubwa, moja kwa jili yake mwenyewe na jingine kwa ajili ya babaye Tedi, Andrea. Bila kusita, Jami akaanza kukata mti wa kwanza mkubwa uliokuwa jirani yake. Andrea akafuata mkumbo. Mara hewa ikajaa harufu ya utomvu wa miti na jasho. Wakati miti ilipoanguka, Jami aliwambia wanakijiji kuondoa nyasi na matawi katika eneo lile ili kuzuia hatari ya moto kichaa. Baada ya hapo, wakakata miti waliyoiangusha katika magogo mafupi na kuyapanga moja juu ya jingine. Mianya kati ya gogo na gogo ikazibwa kwa matawi madogo.
Taratibu, lundo la magogo lenye rangi ya shaba likatokea.
“Sasa tunafunika magogo ya miti kwa udongo,” Jami akaelekeza.
Wanakijiji wote wakachukua makoleo na kulundika tabaka kubwa la udongo juu ya yale magogo ya miti mpaka ikawa kama mlima mdogo wenye rangi ya shaba.
“Barabara!” Jami akapaza sauti kwa furaha. Akawatazama kwa majivuno wanafunzi wake waliokuwa wakifanya kazi kwa bidii.
“Sasa tunauwasha moto mlima huu!”
Kwa haraka, Jami akapanda juu ya mlima ule na kuwasha moto yale magogo ya miti.
“Magogo haya hayatateketea yote kwa moto”, Jami alifafanua. “Yatabadilika kuwa mkaa kwa sababu undongo na nyasi tulizofunikia magogo hayo vinahakikisha kuwa kiasi kidogo tu cha oksijeni kinafikia moto unaounguza magogo”.
“Huu mlima unaitwaje?” aliuliza Tedi kwa aibu. Alikuwa amejificha nyuma ya vazi malidadi la mama yake leye rangi ya bluu.
“Unaitwa tanuri, msichana mpendwa”, Jami akasema.



## Zama za mkaa

Uchomaji mkaa ulilijaza anga la Mtakuja kwa harufu ya miti iliyochomwa, utomvu wa miti na majani mabichi yaliyokatwa. Kila mchoma mkaa alikata miti yake, akatengeneza tanuri lake na kuchoma mkaa wake. Hali hii ikapelekea kuwa na mtawanyiko wa hapa na pale wa maeneo ya wazi mithili ya mashimo yaliyokatwa miti na yale yaliyobaki na miti katika msitu. Katika maeneo yaliyokatwa miti kulisalia visiki vingi, ambapo, mara chache visiki vilichipua na kuzalisha mashina na matawi ya miti mipya. Baada ya muda, baadhi ya mashina na matawi hayo ya miti yaliweza kukua na kuwa miti mipya mikubwa. Na wakati mwingine, visiki vilibakia kuwa visiki bila kuchipua na miti ikapotea Mabaki ya matanuri yaliweka taswira kama makovu katika ardhi ya msitu, ikiwa na udongo mtupu na mabaki ya vipande vya mkaa.

“Kuwa makini Tedi! Kabla hujajua lolote, ndezi watadhani msitu wetu umegeuka kuwa jibini iliyojaa matundu!” Andrea alipaza sauti.
Akaangua kicheko kikianzia katika tumbo lake la kitambi na kuishia katika sharubu zake ndefu.
“Siwezi kuchelewa, baba!” Tedi alijibu. “Nawapenda ndezi. Lakini nina uhakika wao wangependa kula ule ugali wako mkubwa wa kila asubuhi.”

Jami alinunua mkaa kutoka kwa wanakijiji na kuusafirisha kwenda mji ule mkubwa kwa kutumia pikipiki yake nyekundu ya thamani. Njiani aliacha michirizi ya vumbi na vipande vya mkaa. Aliuza mkaa katika soko lilosheheni viungo vya vyakula, matunda na watu waliovaa nguo zenye rangi za kung’aa. Kila mara Jami alipofika sokoni, wateja wa mkaa walimzunguka kama kundi la nyuki likitafuta maua. “Njooni muone ndungu zangu, njooni mguse, njooni mnuse!” Jami alipiga kelele kwa nguvu zaidi ya muuzaji yeyote aliyewahi kuishi.
“Tazama mkaa bora duniani kote. Umetengenezwa kwa miti ile mizuri katika nchi hii.”
“Tunajua hayo Jami” wateja wakapaza sauti. “Ni mkaa bora ambao tulikuwa hatujawahi kutumia. Tafadhali tuletee zaidi!” “Haya, haya, matamanio yenu ni kama amri kwangu” alijibu Jami na akarudi Mtakuja kwa haraka alivyoweza.
“Watu wa mjini wanapenda mkaa wenu, ndugu wanakijiji” Jami alipaza sauti.
“Tafadhali tengenezeni mkaa zaidi!”
Wanakijiji wakabeba mashoka na makoleo yao wakaelekea msituni. Walifurahi kwa kuwa haikuwa shida tena kuwa na chakula mezani kwao.

Taratibu lakini kwa hakika maeneo ya wazi kama matundu yakazidi kujitokeza kwa wingi katika msitu
.



## Nyakati nzuri katika Mtakuja

Tedi, Andrea, Lea na Jami wakakaa pamoja chini ya anga la jioni lenye rangi ya machungwa. Walitafuna matunda na karanga wakati Jami alipowaburudisha kwa simulizi zake kuhusu mji ule mkubwa. “Jana ndugu zangu”, alisema, “watu milioni moja walinizunguka kule sokoni. Naapa. Mimi ni mtu maarufu zaidi katika mji ule!”
Andrea akacheka kwa sauti huku akimpigapiga Jami mabegani.
“Tunakuamini, Jami,” alisema. “Tunakushukuru, kwa sasa tuna hela za kutosha kumlipia Tedi ada ya shule. Kesho ni siku yake ya kuanza masomo.”
Tedi alishindwa kujizuia kutabasamu. Alikuwa mwenye furaha isiyo na kifani.
“Asante mama, baba na Jami,” Tedi alisema. Akawakumbatia wote kwa pamoja.
“Mmeifanya ndoto yangu itimie!”

Kesho yake, Tedi alikaribishwa shuleni. Mwalimu, Bi Rashida, alikuwa mwanamke mkarimu lakini mkali, alivaa kilemba cha rangi ya kijani kilichong’aa mithili ya vitabu vyake. Kwanza, Bi. Rashida aliwafundisha herufi, kisha maneno, kisha namba. Wakati kila mmoja alipokuwa amechoka, aliruka juu!
“Ngoja niwasimulie hadithi!”
“Tedi,” Bi Rashida alisema, “waweza kuleta kile kitabu cha wanyama wadogo waishio katika ardhi, tafadhali?”
Kwa haraka Tedi akatembea kuelekea ile kabati kubwa sana ya vitabu iliyosimama katikati ya darasa. Vitabu vilitoa harufu kama ya maelfu ya siri zikisubiri kugunduliwa. Wanafunzi wote wakakusanyika juu ya zulia na mito ya sofa yenye rangi za kuvutia katika kona ya darasa iliyokuwa na utulivu, ambapo Bi Rashida aliwasimulia hadithi kuhusu wanyama wengi wadogo-wadogo waishio ardhini.
Kila mmoja aliishangaa sakafu iliyokuwa chini yao na kuitazama kwa shauku.
“Wendawazimu nyingi, hamwezi kufikiri?” alinong’ona mvulana aliyeitwa Teo, aliyekaa karibu na Tedi. “Dhana ya mamilioni ya wanyama wadogo kuishi chini ya nyayo zetu”. “Siyo tu chini ya nyayo zako Teo”, alisema msichana aitwaye Roza.
“Namwona mmoja katika nywele zako!”
“Ovyo! Unaye mmoja nyuma ya sikio lako ewe msichana mwendawazimu” Teo alijibu.
“Aliye kwako anatisha ewe mvulana mwendawazimu!” yule msichana aling’aka.
Mara akamsogelea na kumfinya tumbo Teo mpaka wote wawili walipogalagala ardhini kwa kichecko.
“KIMYA”, Bi Rashida akawafokea.
“Roza na Teo, mambo gani hayo mnafanya?
“Tunaigiza kuwa kama wanyama wa ardhini, Bibi!” alisema Roza huku akiwa amekaza macho. Akafunga vizuri kitambaa chake cha kichwani.
“Haya, wanafunzi, kama mnavyoweza kuona, tumepata wanyama wawili wapya ambao bado hawajaelezwa katika kitabu chenu!” Bi Rashida alisema. Inatupasa kuwambia wandishi.”
Wanafunzi wakaangua kicheko. Bi Rashida akacheka kimya kimya.

Tedi akawatazama wale wanyama wawili wa ardhini wenye wazimu waliokuwa karibu yake na akatabasamu.
“Natumaini tutakuwa marafiki wa wazuri”, alifikiri."


2+2=4

## Tedi aenda chuo kikuu

Tedi, Teo na Roza walifanya vizuri sana shuleni kiasi kwamba walipewa tuzo toka serikalini. Hii iliwawezesha kupata ufadhili wa kusoma bure katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, moja ya vyuo vikuu bora nchini. Tedi alipopata taarifa hizo, alikimbia haraka kwenda msituni na akacheza pamoja na Tembo huku na kule msituni mpaka wakanguka chini. Ghafla tabasamu kuu la Tedi likatoweka na machozi yakamlengalenga katika macho yake. Chuo kikuu hicho kilikuwa mbali toka Mtakuja. Hii ilimanisha asingeonana na wazazi wake na Tembo kwa muda mrefu.

“Tutaonana baada ya miaka mitano, Tembo,” Tedi alisema, huku akiwa ameukumbatia kwa nguvu mkonga wa tembo uliojaa makunyanzi. “Naomba unitunzie wazazi wangu.”

Tembo akapepesa macho yake yaliyo mithili ya zabibu.

“Tuutuut!”

“Najua hiyo ‘tuutuut’ Tembo”, Tedi alisema. “Inamaanisha, nakusikia. Sasa achana na mimi, unanibana pumzi ewe msichana mwenye wazimu, siyo?”

Tembo akapepesa macho. Tedi akacheka mpaka akatoa machozi.

“Nitakukosa , Tembo!” Tedi akalia.

“Tuut!”

Tedi, Roza na Teo walisafiri umbali mrefu kwenda chuo kikuu, wakapita katikati ya milima mikubwa, wakavuka mito yenye dhoruba, na wakapita maeneo yenye madimbwi yenye harufu ya uvundo. Hatimaye walipowasili, walipokelewa na Mshauri wa Wanafunzi wa chuo kikuu. Moja ya kazi za Mshauri wa Wanafunzi ilikuwa kuwasaidia wanafunzi kuchagua fani za masomo wazipendazo zaidi.

“Karibuni!”, Mshauri wa Wanafunzi alisema. “Mgenpenda kusomea masomo ya fani gani?”

“Napenda watu, Roza alisema. “Sisi ni viumbe wa ajabu, wacheshi na wakarimu. Nataka kujifunza kila kitu kuhusu watu na kwa nini tunakuwa na tabia tulizonazo.”

“Inafurahisha! ‘Sosholojia’ ndiyo fani yako” Mshauri wa Wanafunzi alijibu.

“Vipi kuhusu wewe, Tedi,” Msahuri wa Wanafunzi alisema “Napenda msitu na wanyama wote washio humo,” Tedi alisema. “Ningependa kujifunza namna tunavyoweza kuwalinda.”Macho yake ya ndoto yalijaa upendo kwa viumbe hai vyote vilivyopo kwenye uso wa dunia.

“Ni ajabu! ‘Misitu’ ndiyo fani inayokufaa!” Mshauri wa Wanafunzi alijibu.

“Hii ni nzuri, Tedi!” Teo alisema. Akampa tabasamu kubwa na akamgusa mabegani taratibu.

Tedi akaona haya anakaangalia chini kwenye miguu yake. Roza akatabasamu na kukenua.

“Acha utani na utwambie ni fani gani unayopenda kusomea Teo,”Roza alisema.

“Ningependa kuwa kiongozi wa kijiji mara kiongozi wetu atakapostaafu,” Teo alisema. Ghafla macho yake ya uchangamfu yakabadilika kuwa ya mtu mwenye kumaanisha. Alijua kwamba kuwa kiongozi wa kijiji kunambatana na majukumu mazito.

“Ajabu!”, alisema Mshauri wa Wanafunzi. “Utawala wa uma’ ndiyo fani yako ya masomo”.

Na hivyo Tedi, Roza na Teo kila mmoja akaelekea njia yake. Kila mmoja wao alisomea fani ya masomo iliyomvutia zaidi. Hata hivyo waliendelea kuwa na mawasiliano ya karibu. Kila wiki walikutana na kunywa kahawa pamoja katika mgahawa wa kifahari wa chuo kikuu ulioendeshwa na mwanamke mrembo ambaye vikombe vyake vya rangi ya pinki vilitamanisha kunywa kahawa pale. Nyakati za mwisho wa wiki walifanya ziara za matukio katika milima mikubwa ya kuvutia iliyozunguka chuo kikuu. Wakiwa njiani katika ziara hizo waliongea wao kwa wao kuhusu mambo waliyokuwa wamejifunza.


University
Chuo Kikuu

## Tedi arudi Mtakuja

Baada ya miaka mitano ya masomo, Tedi alirudi nyumbani. Mabutu ya yake mawili katika nywele zake yalikuwa yameongezeka na kuinuka juu zaidi katika kichwa chake. Alikuwa na shauku ya kukimbia tena msituni pamoja na Tembo na kubadilishana simulizi ya habari na wazazi wake. Angeweza kuwambia mambo yote kuhusu ziara zake za chuo kikuu nao wangeweza kumwambia kuhusu harakati za siku hadi siku za Mtakuja. Tedi alipiga mluzi kwa matumaini. Wakati wowote, alitarajia harufu ya majani na miti ijaze pua zake.

Lakini alipofika katika ukingo wa msitu miguu ikashindwa kutembea na pumzi ikabana. Akabaki mdomo wazi. Mahali palipoota miti mikubwa zamani, palibakiwa na visiki tu. Mamia ya visiki yalifunika ardhi, mithili ya mawe ya makabuli katika viwanja vya maziko. Mahali ambapo awali ziliota nyasi na mimea na maua, sasa palibakia na mchanga ambao ulipeperuka hata kwa upepo mwepesi tu.

Hatua za Tedi zilizokuwa na furaha zikageuka kuwa hatua za kushuhudia miti iliyokatwa, wakati alipotembea kukatisha ardhi tupu isiyo na uoto wowote katika eneo ambalo awali lilikuwa na msitu. Aliwakuta wazazi wake wakiwa wamejiegemeza kwenye nyumba yao kwa huzuni. Baba yake alikuwa ameshapoteza kitambi na ncha za sharubu zake hazikuwa zimejisokota kama zamani. Mama yake bado alionekana malidadi kama zamani lakini mashavu yake yalikuwa yamenywea na kupauka.
“Tedi!” walisema. “tunayofuraha kubwa kukuona. Namna ulivyokua! Tuambie yote kuhusu ziara zako za chuo kikuu.” Tedi akawakumbatia kwa nguvu.
“Kulitokea nini?” aliuliza.
Wazazi wake wakatazamana wao kwa wao. Walisita, hawakuwa na uhakika waanzie wapi.
“Tulibadilisha miti kuwa mkaa kwa kasi ya haraka kuliko uwezo wa msitu kuota na kurejea na hivyo tukaharibu msitu wetu,” Hatimaye Lea alisema. “Hatukuwa na chaguo jingine. Tulihitaji kipato ili kuishi. Pole sana Tedi, lakini ule mti wa mwisho ulipokatwa hata Tembo naye akatoweka”.
Baada ya kusikia taarifa hizo mabutu ya nywele za Tedi yakanywea na machozi yakatiririka hadi miguuni pake kiasi cha kulowanisha eneo la ardhi alipokuwa amekanyanga.
“Tunafanyaje sasa?” Tedi aliuliza.
”Hatujui, Tedi”, mama yake akajibu kwa huzuni. “Imekuwa hata vigumu kwetu sasa kuzalisha chakula katika mashamba yetu kwa sababu upepo uvumapo hupeperusha udongo wote wenye rutuba. Chakula kimekuwa haba.” “Inaonekana hakuna tumaini tena,” baba yake aliongeza.
Hofu ikajaza moyo wa Tedi.



## Tedi achukua hatua

Siku moja baada ya kuwasili Tedi alikwenda kuwatafuta Roza na Teo.
“Nina mpango!” Tedi akawambia. Ndani ya macho yake palikuwa kama moto kichaa badala ya utu wema kama kawaida yake.
“Tuwaite wanakijiji wote pamoja!”
Wanakijiji wakajisogeza katika uwanja wa mikutano. Miamba magumu ilichukua nafasi ya mahali ambapo awali palifunikwa na nyasi na mchanga laini. Macho ya watu wote yalielekea kwa Tedi, aliyekuwa amesimama katikati ya uwanja wa mikutano mithili ya malaika wa vita nyakati za vita.
“Mimea yote na wanyama katika msitu vinategemeana,” Tedi akafafanua kwa wanakijiji. “Kwa kukata miti mingi kupita kiasi, tuliondoa makazi ya wanyama. Wakati huo huo, upepo na mvua vikasomba udongo wote wenye rutuba ambao mimea na miti vinahitaji ili kuota. Sasa ni vigumu kwetu kuzalisha chakula na msitu kurejea tena.” Wanakijiji wote wakainamisha vichwa vyao. Upepo ukavuma kuwazunguka, ukabadilisha anga kuwa la vumbi la kijivu.
“Kwa bahati nzuri, nimejifunza kuhusu njia tunazoweza kutumia kurejesha msitu wetu” Tedi akasema.
“Pia najua namna tunavyoweza kulinda msitu wetu siku za baadaye,” Tedi akaongeza. “Kama tukifanya kazi kwa pamoja, nina uhakika kuwa msitu utarudi! Yamkini tunaweza hata kurudia kuchoma mkaa tena. Kwa msaada wenu, kiasi kikubwa cha msitu kitarejea tena baada ya muda. Nina uhakika huo!”
Wanakijiji wakatazamana. Inawezekanaje tena kubadilisha jangwa hili la mwamba kuwa msitu wa miujiza tena? Tedi akainua kichwa chake juu.
“Tazameni!” alisema. “Kama mkiangalia kwa makini visiki vilivyoachwa katika uwanda huu, mtaona baadhi vikiwa vina mashina na matawi madogo madogo. Baada ya muda, hayo mashina na matawi yatakua na kuwa miti mipya. Namna hii ya kuota mashina na matawi kwenye visiki hujulikana kitalaamu kama ‘uchipushaji’. Mnaweza pia kuona vitoto vidogo vya miti hapa na pale. Hii inamaanisha msitu wetu tayari umeanza kurudi!”
Wanakijiji wakatazama pande zote. Hakika, wakafikiri. Kuna miti michanga na visiki vinavyochipua katika eneo lote linalotuzunguka.

“Mngependa kunisaidia kurejesha msitu?” Tedi akauliza.
Minong’ono ikaanza miongoni mwa wanakijiji wa Mtakuja. Kisha wazazi wa Tedi wakajitokeza mbele.
“Tupo tayari!” wakasema, wakimtazama binti yao kwa majivuno makubwa.
“Tupo tayari pia!” wanakijiji wakaunga mkono.
Mwishowe, kiongozi wa kijiji akasimama kutoka katika stuli yake ya mbao iliyokuwa imechongewa taswira za ndege, miti na nyani mjuvi. Makunyanzi ya paji la uso wake yalikuwa yameongezeka kina. Mgongo wake nao ulikuwa umepinda kutokana na matatizo yaliyokikumba kijiji chake.
“Asante Tedi,” akasema. “Tuna imani na wewe. Nitakusaidia kurejesha msitu katika miaka ijayo.”
“Tunaweza kufanya jambo hilo!” wakaunga mkono wanakijiji.
Tedi akangalia umati ule kwa shukrani. Alifurahi kuona matumaini yakirudi katika macho ya watu.
“Ndiyo tunaweza” akapaza sauti.



## Mkutano wa kijiji

"Teo," Tedi alisema huku akipunga mkono kwa upole, "tuambie kuhusu uongozi. Tunahitaji kutunga sheria zipi kuhakikisha hatukati miti mingi kupita kiasi tena?"
Teo akatazama vichwa vingi vya watu vilivyomwelekea katika uwanja wa mikutano na akavuta pumzi kwa kina. Hii ilikuwa ni fursa yake kufanyia kazi ujuzi wake wa uongozi.
"Jambo la muhimu zaidi ni kuhakikisha kila mmoja anaalikwa kusaidia katika kutunga sheria hizo," Teo alisema. "Kutakuwa na uwezekano mkubwa zaidi sisi kufuata sheria tutakazokubaliana kwa pamoja. Kwa mfano, kama kila mmoja akikubali kwamba mtu achome magunia matano tu ya mkaa kwa mwaka, kila mmoja atakuwa na uwezekano wa kufanya hivyo."
Kiongozi wa kijiji akaruka toka kwenye stuli yake kwa shauku.
"Kumbukeni kuwa tayari huwa tunafanya maamuzi kwa pamoja" alisema. "Kila mwezi, huwa tunaongea kwa pamoja hukusu mashamba yetu na kufanya maamuzi kuhusu mazao gani ya kupanda na wakati gani tuvune. Tunachohitaji ni kujumuisha misitu katika mazungumzo yetu ya namna hiyo!"
"Hili ni wazo bora Teo, hakika ni wazo bora," kiongozi wa kijiji akaongeza.
Moyo wa Teo ukalipuka kwa kiburi. Akatabasamu sana akimtazama Tedi, aliyekuwa amesimama pembeni karibu yake. Alipokutanisha macho na Tedi, tumbo la Tedi likawa kana kwamba limejaa vipepeo wa rangi ya bluu na njano. "Usije ukapoteza mwelekeo sasa!" Tedi akajiambia moyoni. "Tupo katika kazi maalumu ya kuokoa kijiji na sasa niwaze juu ya mvulana tu!"

Kwa haraka Tedi akarejesha fahamu zake. "Roza!" Tedi alisema, akitabasamu kwa uchangamfu dhidi ya rafiki yake. "Ni njia gani nzuri tunayoweza kutumia ili kufanya kazi kwa pamoja kurejesha msitu wetu?" "Swali zuri, Tedi," Roza alisema. Akasimama huku ametanua miguu yake mbele ya wanakijiji mikono yake akiwa ameshika nyonga. Kilemba chake cha rangi ya pinki kilipepea kwa upepo.
"Kuna njia nyingi tunaweza kutumia kufanya kazi pamoja," Roza akaanza. "Tunaweza kuunda vikundi vya walinzi wa msitu, wapandaji wa miti na wachoma mkaa ambavyo vinakutana kila mwezi. Katika mikutano hiyo, vikundi vinaweza kuamua namna ya kulinda miti michanga na miti inayochipua dhidi ya uharibifu wa ng'ombe wanaolisha na mioto kichaa. Vikundi vinaweza pia kuweka mipango ya maeneo ya kupanda miti na kiasi cha mkaa cha kuzalisha. Kila mwenye nia ataweza kuwa tayari kujiunga na kikundi kimoja wapo, ili kwamba kila mmoja aweze kusikiwa na mawazo yote yaweze kukusanywa!"

Tedi akasimama juu.
"Hivyo, tunachohitaji kufanya ni kumshirikisha kila mmoja, kukutana mara kwa mara na kushirikishana mawazo yetu," Tedi alisema.
"Rahisi kama uji na mgonjwa!"
Wanakijiji wakaangua kicheko. Kwa kicheko hicho wanakijiji wakaondoa msongo wa mawazo walioupata katika miaka ya nyuma. Kila mmoja akaanza kusemezana na mwenzake kwa furaha. Kiongozi wa kijiji akatabasamu. Alijua changamoto nyingi zingetokea mbeleni, lakini akabaki na wasiwasi wake moyoni. Kwa upendo akaweka mkono wake juu ya mabega ya Tedi, akiwa amevutiwa sana na ujasiri mkubwa wa msichana huyo.
"Na itakuwa rahisi kama uji na mgonjwa!" alisema.



## Wanakijiji waandaa mpango

Kesho yake wanakijiji wote wakakusanyika katika darasa la kijiji kuunda mpango wa kurejesha msitu. “Wazo langu ni kuweka lebo kwenye kila gunia la mkaa,” Mohamedi alisema. “Wale watakaofuata sheria watapata lebo. Kwa njia hii tutaweza kuona kama watu wanafuata sheria na tunaweza kufuatilia mkaa wetu kuanzia hapa hadi ule mji mkubwa.

“Hebu tuweke lebo yetu iwe ‘Nishati ya Tedi’!” Andrea alipendekeza huku akimwangalia bintiye kwa kujivuna.

“Ndiyo!” wanakijiji wote wakatikisa vichwa kwa shauku. “Barabara kabisa.”

“Napenda wazo hilo, lakini tunahitaji miti ili kuchoma mkaa,” mmoja wa wanakijiji akatoa angalizo. “Tutawezaje kurejesha miti? Na muhimu zaidi, itachukua muda gani kabla kutujaanza kuchoma mkaa tena?”

“Tedi!”, Roza na Teo, walisema kwa pamoja. “Tunakuhitaji!”

Tedi akatambaa toka nyuma ya daftari lake la kipepeo na kutembea kwenda mbele ya darasa. Mikono yake na vazi lake vilikuwa vimetapakaa mamilioni ya matone ya wino. “Miti inahitaji muda kukua,” Tedi alisema. “Baada ya miaka mitano, tunaweza kuanza kuchoma mkaa kiasi kutoka kwenye miti tutakayokuwa tumepanda mashambani mwetu. Lakini itachukua takribani miaka ishirini hadi thelathini kabla miti ya msitu wa asili kufikia ukubwa wa kuweza kukatwa kwa ajili ya kuchoma mkaa.”

“Miaka ishirini hadi thelathini!” wanakijiji wakang’aka. “Hiyo ni miaka mingi sana!”

“Kurejesha miti, tunahitaji kupanga pamoja,” Tedi alisema. Akaenda kwenye ubao mkuukuu na kuchora duara kubwa lenye duara dogo ndani yake na nukta katikati ya duara dogo.

“Hebu tuseme duara hili kubwa ni msitu wetu mpya,” alisema. “Duara dogo ya ndani ni mashamba yetu na hii nukta ni katikati ya Kijiji cha Mtakuja. Ni wapi na kwa namna gani mngependa kuchoma mkaa?”

Wanakijiji wakawa kimya kwa muda. Kisha wazee watano marafiki waitwao Yona, Rashidi, Mario, Ali na Azizi, wakaanza kuongea kwa pamoja.

“Hebu tulinde miti michanga na visiki vinavyochipua dhidi ya moto na ng’ombe wanaolisha,” Yona alisema. “Vinginevyo haitaweza kukua na kuwa miti mikubwa.”

“Hebu tuchome mkaa katika eneo hili la ‘miti ya kupandwa ya mkaa’, ambalo watu wote wa Mtakuja watalitunza kwa pamoja,” Ali akaongeza. Akachukua choki na kuchora kwa makini ‘ukanda wa kuchoma mkaa’, yaani eneo ndani ya msitu ambalo lingeweza kutumika kuchoma mkaa mara msitu utakapokuwa umerejea.

“Hebu tuchome mkaa katika miraba midogo ambayo tunaweza kurudia kuivuna kila baada ya miaka ishirini na tano,” Rashidi alisema. Akachukua chaki kutoka kwa Yona na akagawa ‘ukanda wa kuchoma mkaa’ katika miraba. “Hebu tukate miti yenye urefu wa zaidi ya mita mbili tu,” Mario akaongeza. “Hatutaki kuchoma moto watoto wa msitu!” Wanakijiji walicheka.

“Hebu tupade miti mingi pamoja,” Azizi alisema. “Tuna mbegu kiasi tulizoachiwa na mababu zetu. Walitufundisha namna ya kuzipanda. Sasa tu ndiyo nagundua kuwa tayari tulikuwa na maarifa yote tuliyohitaji kurejesha msitu wetu! Tulihitaji kukumbushwa tu.”

Tedi hakuweza kujizuia kutabasamu kwa bidii na maarifa mengi yaliyokuwepo. Teo akamfinya mkono wake.

“Tazama mafanikio haya uliyopata, ewe mpenda ndoto za mchana!” alisema.



## Wanakijiji waotesha msitu

Katika miaka iliyofuata, wanakijiji wote wakasaidia shughuli za kuotesha na kulinda msitu. Walijenga juu ya ujuzi wa jadi waliopokea toka kizazi hadi kizazi. Timu maalumu ya wanakijiji ikalinda miti michanga na visiki vinavyochipua dhidi ya mioto kichaa na ng'ombe walishao. Hii ikatoa fursa ya msitu kurejea kwa njia asilia. Wanakijiji wengine walipanda miti mashambani kwa pamoja. Katika msitu walipanda miti ya mikangazi na migunga na mininga, ambayo ikafanyika kuwa makazi kwa aina mbalimbali za wanyama wa porini. Katika mashamba yao, wanakijiji walipanda miembe na mikorosho na mikwaju. Baada ya muda mfupi miti hii ingeweza kuwapatia chakula, miti ya kujengea na mkaa. Wanakijiji walipata sehemu kubwa ya mbegu za miti walizohitaji toka kwenye 'hifadhi ya mbegu' ya ndani ya eneo lao, mahali ambapo mbegu za misitu hutunzwa kwa makini na kuuzwa na wapandaji miti wenye ujuzi.

"Kupanda miti katikati ya safu za mazao kunahakikisha kuwa udongo hausombwi na mvua inaponyesha," Tedi alimweleza Teo. Teo alikuwa katika mafunzo ya kiongozi wa kijiji mtarajiwa na alijaribu kujifunza kila alichoweza kuhusu kijiji chake.

"Wakati huo huo, miti hutoa matunda, kivuli, na baada ya muda, hata miti ya kujengea nyumba! Miti huufanya undongo kuwa na rutuba, hivyo mazao yanaweza kustawi na kukua haraka katika udongo huo." "Hivyo kimsingi, tunageuza mashamba yetu kuwa mashamba-misitu?" Teo aliuliza.

"Hakika", Roza alisema. Akaegesha mikono yake juu ya mabega ya Tedi na Teo. Kwa pamoja wakatazama ardhi ya kijiji iliyojaa watoto wa miti wengi na visiki vinavyochipua.

"Mashamba-msitu ya namna hii yatatupatia aina nyingi za vyakula na kipato. Kama tukikosa mavuno kwenye nyanya, tutakuwa bado na maembe na mahindi. Kama miembe yetu isipotoa mavuno, bado tutakuwa na ngano na pilipili. Na kama vyote visipozaa bado tunaweza kuchoma mkaa toka kwenye miti." "Nimeelewa", Teo alisema. "Hekima sana!"

Baada ya miaka mitano ya kufanya kazi kwa bidii, msitu akaanza kutokea tena taratibu. Kwa uangalifu wanakijiji wakaanza kuchoma mkaa kidogo kidogo kutoka katika miti ya mashambani mwao. Miaka miwili baada ya kukata miti ya mashambani, miti ile inaliyochipua ilitoa mkaa mpya tena. Baada ya miaka kumi, wakulima wa Mtakuja wakavuna mvuno wa kwanza wa maembe kutoka katika ardhi yao.

"Yamu!" Teo alisema, akiashiria kuridhika kumeza vipande vya maembe yaliyonona.

Teo aliangalia sehemu ndogo ya shamba-msitu waliyokuwa wakiitunza huku Tedi akiwa amelaza kichwa chake juu ya mabega yake. Watoto wa kiume wawili walionekana wakitikisa mahindi shambani, wakijaribu kukamata kuku waliokuwa katika hali ya kuogopa. Teo akabusu nyusi za Tedi.

"Nadhani tunakaribia kukamilisha, Tedi," alisema. Tabasamu la Tedi likageuka kuwa kicheko pale kichwa cha mumewe kilipoangukia begani mwake. Mume wake akaachama na ndani ya sekunde akatoa sauti mithili ya kundi la nguruwe pori.

"Tunakaribia kumaliza", Tedi akanong'ona. "Siwezi kuamini!"

Bado, haikuwa rahisi kama uji na mgonjwa. Ni kinyume chake. Wanakijiji wengi bado walikuwa wakipambana kuweka chakula mezani. Lakini kule kurudi kwa msitu taratibu kulikuwa kumejaza matumaini katika mioyo yao. Punde si punde wangeanza kuchoma mkaa tena toka katika msitu wao wa asili.

"Inawezekana!" wanakijiji wakasemezana wao kwa wao.

"Nyakati nzuri zitarejea tena!"



## Nyakati nzuri zarejea

Miaka mingine kumi ikapita, kisha ishirini. Baada ya muda, wanakijiji wakazidi kubobea katika kutunza msitu wao na miti katika mashamba yao. Walikuwa na chakula zaidi kwa ajili ya kula na kipato zaidi kwa ajili ya kuweka akiba kuliko ilivyowahi kutokea. Rafiki yao mzuri Jami alifurahi. Ingawa wanakijiji wa Mtakuja hawakuwa wamewahi kumlaumu Jami kwa uharibifu wa msitu, alijihisi kana kwamba ilikuwa kosa lake. Kwa miaka ishirini iliyopita, aligeuka kauka nikuvae, mara zote akawa anavaa suti za kijivu na kwa kiasi kikubwa alikuwa amepoteza uchangamfu na masihara yake.

“Nasikitika sana kwa yaliyotokea katika kijiji hiki,” alisema akirudia tena na tena. “Kamwe sitauza mkaa tena.”

Lakini wanakijiji walimpigapinga mabegani mwake, wakamshika mkono na kumpigapiga mgongoni pia. “Kamwe wala usifikirie kutuacha, Jami!” kiongozi wa kijiji alimwambia. “Sisi tunawajibika kwa kutoweka kwa misitu yetu. Ulituletea fursa. Hatukujua tu namna ya kutumia fursa hiyo kwa uangalifu. Punde si punde uchomaji mkaa utashamiri tena. Subiri uone tu!” Macho ya Jami yakajawa nuru na baadhi ya utu wake wa awali ukarejea. “Asante, kiongozi wa kijiji, kwa maneno yako ya hekima na kwa kuamini katika wema wa mfanyabiashara mwenye ujuzi kama mimi.”

Kiongozi wa kijiji alikuwa sahihi. Biashara ya mkaa ilishamiri tena. Ingawa miti katika msitu wa asili haikuwa mikubwa kama zamani, bado iliwezekana kuitumia kuchoma mkaa. Katika msitu, wanakijiji walichoma mkaa ndani ya ukanda wa kuchoma mkaa tu ambao awali Ali alichora katika ramani ubaoni. Walichagua na kukata aina ile ya miti inayotoa mkaa bora. Wakati huo huo, katika mashamba yao wachoma mkaa toka miti michache tu. Miti iliyosalia mashambani ilisaidia kuhifadhi udongo na kutoa matunda na kivuli. Aidha, wanakijiji waliboresha matanuri yao ya kuchomea mkaa. Sasa wakawa kwanza wanakausha miti ya kuchomea mkaa ili kuongeza ubora wa mkaa na pia wakaweka bomba la kutolea moshi kwenye kila tanuri. Haikuchukua muda mrefu kabla wale nyuki wenye rangi nzuri na shughuli nyingi hawajajazana kuzingira eneo Jami alikouzia mkaa kule sokoni kwa mara nyingine tena.

“Njooni mjionee!” “Njooni mguse!” “Njooni mnuse!” Jami alifurahia. “Huu ni mkaa endelevu nchini kwa mara ya kwanza! “Nishati ya Tedi siyo tu mkaa wenye ubora, bali unaokoa misitu pia. Kiasi kidogo cha hela unayolipia mkaa kwa mifuko hii ya mkaa kinaenda moja kwa moja kwa wanakijiji wa Mtakuja. Wanakijiji wanatumia hela hizo kupanda miti zaidi. Maneja wetu wa msitu, Tedi, ameweka utaratibu mzuri na anadhibiti kila kitu. Angalia, yeye yupo kabla na baada ya msitu wa Mtakuja kutoweka.”

Watu wa ule mji mkubwa wakapata msisimko.

“Ni mwanamke wa mfano wa kuigwa! Mwanamke mkorofi kama nini! Miti ya ajabu kama nini! Ndege-Tausi wazuri kama nini! Maembe bora kama nini!


Wateja wa Nishati ya Tedi walirejea nyumbani wakiwa na nyuso za tabasamu. Huko wakapika milo yenye ladha zaidi kwa ajili ya marafiki na familia zao.


Tedd
Teddy's
Teddy
Teddy's
Teddy's Energy
Teddy's
Energy
Teddy's
Energy

## Kipingamizi

Wakati wa maazimisho ya awamu ya hamsini ya siku ya kuzaliwa Tedi, wanakijiji wote wa Mtakuja walikusanyika kwenye uwanja wa mikutano, ambao kwa mara nyingine ulikuwa umefunikwa tena na nyasi laini na majani. Tedi alikuwa amefichwa na watoto wake wavulana wadogo waliokuwa wamemkumbatia kwa nguvu, ambao wakati huo walionekana kuwazidi urefu wazazi wao mithili ya twiga waliokua.
“Heri ya siku ya kuzaliwa mama!” mwanaye wa kiume alisema.
“Asante wavulana.” Tedi alitabasamu.
Ghafla, manung’uniko ya hofu yakaibuka miongoni mwa wanakijiji.
“Ndugu zangu,” Teo alisema. “Rais amepiga marufuku uchomaji wa mkaa.”
“Macho ya Tedi yaliyokuwa katika hali ya kuchanganyikiwa yakakutana na ya Jami, ambaye uso wake ulibadilika na kuwa rangi ya njano kama tai yake. Huku akitetemeka akamkabidhi Tedi gazeti lililokuwa na taarifa hiyo.
Tedi akasoma kwa sauti. “Wananchi wapendwa, uchomaji wa mkaa unaharibu misitu ya nchi yetu. Ili kuzuia uharibifu zaidi, kuanzia sasa uchomaji mkaa utakuwa haramu. Tutanunua gesi toka majirani zetu iwe nishati mbadala ya kupikia. Natarajia kuwa kila mmoja ataacha uchomaji mkaa mara moja. Wasalaamu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.”
Yale mabutu ya nywele za Tedi yaliyokuwa yametuna kwenda juu ya kichwa cha Tedi kwa zaidi ya miaka ishirini, yakanywea tena kwa mara nyingine.

Mara, wanakijiji wote wakakusanyika katika darasa la kijiji kwa mkutano wa dharura. Rashidi na Joni, watoto wa Tedi na Teo, wakawa wa kwanza kuongea. Wote wawili walikuwa wapenzi wa mambo ya siasa. “Ukweli kwamba uchomaji mkaa sasa ni haramu siyo tu tatizo kwetu bali kwa vijiji vingine vingi sana nchini,” Rashidi alisema. Misitu mingi ya majirani zetu ni kama imekwisha haribiwa kabisa. Pia hawawezi kuchoma tena mkaa wowote toka miti iliyo katika mashamba yao. “Hii itawapunguzia kipato kwa kiasi kikubwa na inaweza kuwa ni suala la kufa na kupona kwao.” “Ni lazima tufanye kitu mara hii!” Joni aliongeza. “Nadhani Rais wetu hatambui ni kwa kiasi gani maauzi yake haya yataleta madhara kwa makumi elefu ya wachoma mkaa nchini.” Teo akaitikia kwa kichwa. Kwa kujivuna aliwangalia watoto wao wavulana.
“Umesema vema,” alisema. “Hata hivyo, Rais ana sababu ya kuwa na hofu. Misitu ni makazi ya wanyama wengi wa aina mbalimbali na huzalisha gesi ya oksijeni tunayopumua. Kumbuka adha iliyotupata pindi msitu wetu ulipotoweka. Ardhi ya kijiji chetu iligeuka kuwa jangwa lisilozaa chochote. Kitu cha namna iyo hiyo kinawatokea majirani zetu wengi wakati huu huu. “Rais anatakiwa awalinde wao na misitu yao.”
“Laikini, Rais anasema hatuwezi tena hata kuchoma mkaa kutoka kwenye miti tuliyopanda mashambani mwetu!” Roza akapiga kelele. Akiwa amechemka alirusha mikono yake hewani. Macho yake yalionekana kana kwamba yanafyatua radi.
“Sioni sababu kwa nini uchomaji mkaa upigwe marufuku nchini kote!”
Wanakijiji walianza kupiga kelele wote kwa mara moja.
“Huyu Rais ni balaa!”
“Hapana, anatujali”
“Hawezi kutufanyia hivi!”
“Ndiyo, anaweza!”
“Ni lazima kupinga!”
“Hapana, ni lazima tukubaliane na maamuzi yake!”


Protect our forests
Ban charcoal production
Linda msitu wetu
Piga marufuku uzalishaji wa makaa
President
Rais

## Wazo la kishujaa

Siku iliyofuata, wanakijiji wakakusanyika katika darasa la kijiji kwa mara nyingine. Kila mmoja alikuwa bado akipiga kelele na mayowe wakiongea wao kwa wao. Ilionekana kutokuwa na suluhu ya jambo hilo. Hata Teo hakuweza kuzuia machafuko hayo.
Baada ya saa moja hivi, mtu mmoja alionekana kwa mbali, mithili ya kivuli kidogo, akinyosha mkono kutokea upande wa nyuma.
“Samahani kwa kila mmoja. Samahani mabwana, mabibi. Mnisamehe kwa kuwakatiza maongezi. Nina wazo,” alisema msichana mmoja.
Alitetemeka kuanzia kichwani hadi vidole vya miguu.
Roza, ambaye alikuwa akilitazama kundi mithili ya mwewe, akaruka juu ghafla.
“KIMYA!”, alipiga kelele. Aliwatazama wanakijiji kwa macho makali sana ambayo bila shaka yangemfanya Bi Rashida ajivune.
“Mwacheni Mei aongee.”
“Asante, Roza,” Mei akatamka kwa kigugumizi. Aliweka sawa gauni lake la bluu na akashusha pumzi kwa nguvu. “Nilisomea, ‘ushirikishaji wa umma,” alianza. “Wakati wa masomo yangu, nilijifunza namna nzuri ya kuwasilisha habari ngumu kwa kila mmoja katika nchi kwa namna ambayo kila mtu anaweza kuelewa.”
“Programu ya Nishati ya Tedi,” Mei aliendelea kwa ujasiri zaidi, “ni wazomuhimu.” “Tumeona kuwa inafanya kazi vizuri kwa sababu tunachoma mkaa bila kuharibu msitu wetu. Vipi kama tukiwaambia majirani zetu kuhusu Programu ya Nishati ya Tedi? Vipi kama nao wakitunza misitu yao kama tunavyofanya sisi? Labda misitu ya nchi nzima itarejea, kama vile tu ilivyorejea katika kijiji chetu. Je, hatufikirii kwamba Rais wetu angependezwa na jambo hili?”

“Wazo la hekima!” Tedi alisema. Akatabasamu dhidi ya Mei, akiwa ametiwa moyo na ujasiri wake wa kuongea. “Tunaanzia wapi?”
Wakati huo Mei alimshangaza hata Roza.
“Wazo langu ni kumwalika Rais kijijini kwetu,” Mei alisema kwa upole, macho yake yakiwa yanatazama chini sakafuni.
Ghafla ikawa kana kwamba chumba kimejazwa na kicheko cha kundi la watoto wa miaka mine badala ya watu wazima. Wazo la ukichaa kama nini, wanakijiji waliwaza. Lakini bado, itakuwa kitu cha ajabu kama nini iwapo kweli Rais atakubali kuja hapa!
Jami akaruka juu na kupunga kofia yake juu ya kichwa chake kwa shauku.
“Ni wazo la ajabu Mei! Msihofu ndugu zangu wapendwa!” alisema kwa furaha.
“Najuana na watu wengi katika ule mji mkubwa. Miongoni mwao wamo marafiki wa marafiki wa marafiki wa Rais mwenyewe. Kwa msaada wa kila mmoja katika Mtakuja, Rais atakuja kufanya ziara hapa siku si nyingi! Wote tunajua kuwa Programu ya Nishati ya Tedi inafanya vizuri. Rais anahitaji tu kujionea mwenyewe.” Tedi na Teo wakatazamana. Walijua hapakuwa na cha kupoteza.
“Kama kiongozi wetu alivyowahi kusema miaka iliyopita,” Teo alimwambia Jami. “Tunakuamini Jami. Tuna swali moja tu. Tunaweza kufanya nini ili kukusaidia?”
Jami akataasamu tabasamu la mtu ajuae bayana kinachohitajika kufanyika ili kufanya lisilowezekana liwezekane.
“Nitawaambia asubuhi,” alisema.
“Hebu ngoja tupate usingizi kidogo kwanza. Naamini leo tumetumia nguvu za kutosha kuangazia nchi nzima!”


80x
160x2=

## Mshikamano

Kesho yake, Jami, Tedi, Teo, Rashidi, Joni na Mei walikutana katika darasa la kijiji. Jami alijiamini katika uwezo wake wa kuweza kupanga mkutano na Rais. Lakini alijua kuwa Rais angehitaji kusikia zaidi ya maneno ya ujanja ujanja wa mjini ili kumfanya afunge safari hadi Mtakuja.

“Rashidi, Joni,” Jami alisema. “Namna gani tutaweza kumshawihi Rais kuwa Programu ya Nishati ya Tedi imefanikiwa?”

Joni akajikuna kidevu na kuweka sawa kola ya suti yake ya kijani.

“Anahitaji takwimu, takwimu za kutosha,” Joni alifafanua. “Takwimu ni tarakimu na maelezo. Takwimu lazima zioneshe kuwa tuliotesha misitu yetu. Takwimu lazima zioneshe kuwa tunachoma sehemu ya mkaa wetu toka miti tuliyopanda katika mashamba yetu na kuwa hii inaleta faida ya kuongeza rutuba ya udongo mashambani. Sambamba na hili, ni lazima takwimu zioneshe kuwa tunachoma mkaa bila kuharibu msitu wetu na wala hatuondoi miti yote katika mashamba yetu. Hii itaweza kuonesha kuwa hatujaribiwi tena kuvuna miti zaidi ya uwezo wa kuzalisha kwa misitu yetu ya asili na ile ya mashambani. Hii ni ya ajabu kwa sababu watu katika mji ule mkubwa wanahitaji mkaa zaidi kuliko ilivyowahi kuwa na wanalipa bei nzuri. Mwisho, takwimu lazima zioneshe kwamba kipato chetu kimeongezeka kutokana na kuchoma mkaa na kuwa tunaweza kupeleka watoto wetu shule kutokana na kipato hicho.”

“Ni lazima tuandike matokeo katika taarifa ambayo ni fupi na rahisi kuelewa,” Joni aliongeza. “Wakati huo huo, taarifa hiyo ni lazima ijumuishe habari nyingi kwa kadri inavyowezekana.”

“Ni kama kuweka kurasa elfu moja za taarifa ya kiujuzi ndani ya kurasa kumi,”Rashidi alisema kwa lugha ya kawaida.

“Naamini tuna mchanganyiko wa watu barabara kwa ajili ya shughuli hii,” aliongeza.

“Tedi ataweza kuonesha kuwa msitu wetu umerejea. Roza atatoa dondoo kuwa programu ya Programu ya Nishati ya Tedi inatoa faida nyingi kwa watu. Teo ataweza kuonesha kuwa sheria zinahitajika ili kuhakikisha kuwa watu hawaharibu msitu. Joni na mimi tunajua mambo gani Rais atapenda kujua na kwa nini.”

Rashidi akaegemea kabati la vitabu huku mikono yake ikiwa mifukoni bila wasi wasi kabisa. Aliangalia kwa utulivu uso mmoja baada ya mwingine mpaka hatimaye macho yake yalipotua kwa Mei. Akamkonyeza!

“Na huyu Mei hapa anajua kabisa namna ya kuandika kila kitu ili kila mmoja katika nchi hii aweze kuelewa.” Mei akageuka kuwa mwekundu. Tedi naye akatabasamu dhidi ya utundu wa mwanaye mvulana.

“Nakubali,” Tedi alisema. “Kitu kimoja tu. Hebu tuwaalike wanakijiji watusaidie kuweka mambo sawa. Vinginevyo tutakosa mambo mengi kuhusu ujuzi wao na mawazo yao. Hebu tufanye kazi katika timu. Tutakutana hapa tena baada ya miezi miwili na kuwasilisha matokeo yetu kwa Mei. Baada ya hapo, tutamsaidia aweze kuandika taarifa kwa ajili ya Rais.

Kwa sekunde kadhaa, Macho ya Tedi yalitulia kuangalia ndege waliokuwa wamejenga kiota kwenye tundu moja katika dari la darasa. Kisha akakumbuka mahali alipokuwa.

“Imekubalika?” alisema.

“Imekubalika!” kila mmoja akaitikia, huku wakicheka kwa ile hali ya ndoto za mchana ambayo haikuonekana kumwacha Tedi, bila kujalisha umri wake. “Sawa, tunasubiri nini sasa!” alisema Roza kwa shauku bila kujiuzuia.

“Twende, twende!”


Uchunguzi
miti = 2510
ndege = 32
makaa = 60
wanafunzi = 35

## Kumwalika rais

Katika miezi iliyofuata, timu zile zikakusanya takwimu. Timu zilihesabu idadi ya miti na wanyama na mimea walivyoweza kuviona. Wakaandika kiasi cha mkaa kilichokuwa kimezalishwa na kile kilichokuwa kimeuzwa kwa miaka yote. Wakafanya mahojiano wao kwa wao kujua ni kwa kiwango gani kila mmoja alikuwa anafurahia Programu ya Nishati ya Tedi na faida zilizotokana na programu hiyo. Wakaweka takwimu katika grafu, michoro na maelezo.
Mohamedi alisaidia kupima unene na urefu wa mashina ya miti.

“Tunafanya nini na tarakimu hizi?” alimuuliza Tedi.
“Takwimu hizi zinaweza kutumika kukokotoa kiasi cha wingi wa miti iliyopo na ujazo wake,” Tedi alijibu. “Kiasi cha nishati katika mti kinajulikana kama ‘biomasi’ au ‘tungamotaka’. Biomasi hiyo ndiyo tunayoitumia kuchoma mkaa.”
“Nimeelewa,” Mohamedi alijibu. “Ni muhimu kumwonesha Rais wetu kuwa kuna biomasi ya kutosha katika msitu wetu ambayo tunaweza kutumia kuchoma mkaa. Tunaweza kutumia hizi takwimu kukokotoa hiki.” “Haswa,” Tedi alijibu.
“Lakini kwa nini tunahesabu idadi na aina ya ndege waishio katika msitu wetu,” alisema Azizi, ambaye alitokea kusikia maongezi ya Mohamedi na Tedi. “Idadi kubwa ya aina tofauti za ndege inatujulisha kitu kuhusu kiwango cha uwezo wa msitu kutoa makazi kwa ajili ya wanyama. Msitu wenye afya hutoa makazi kwa aina nyingi za wanayama tofauti tofauti. Wanyama hao ndio hukakikisha mbegu za miti zinasambazwa msituni, hivyo kuwezesha miti mipya kuota. Pia wanyama hao hula majani na sehemu za miti iliyokauka, ambapo kupitia kinyesi chao huongeza rutuba katika udongo. Kwa pamoja wanyama wote na mimea hufanya kazi kwa pamoja kusababisha msitu mzima uweze kuendelea kuwepo katika hali ya utulivu bila mvutano.”
“Sawa!” Azizi alisema. “Hakika Rais atavutiwa sana na hili jambo. Ni vema nianze kuhesabu ndege wengine zaidi!”

Kila mmoja katika kijiji alifanya kazi kwa bidii kukusanya takwimu. Walijifunza mengi kila mmoja kutoka kwa mwenzake, kuhusu msitu na miti ya mashambani kila mahali walipopita. Baada ya miezi miwili, kila mmoja akawasilisha yale aliyogundua kwa Mei, ambaye aliandika taarifa kwa ajili ya Rais.
“Barabara!” Jami alishangaa, baada ya Mei kumkabidhi ile taarifa kwa ajili ya Rais.
“Acha nifanye mazingaombwe yangu!”
Jami akaondoka zake kwa pikipiki yake nyekundu ya kifahali, akawaendea marafiki, wa marafiki, wa marafiki wa yule Rais pekee.

Mwezi mmoja ukapita, miezi miwili ikapita, miezi mitatu mizima ikapita bila kusikia neno toka kwa Jami. Kwa muda wote huo kila mmoja katika kijiji alikuwa akisubiri kwa hamu na kihoro. Hata ndege na mchwa na mbuzi na ng’ombe wa Mtakuja hawakuthubutu kutoa sauti. Kila siku, Teo alikuwa akiiangalia Mtakuja kutokea kwenye kilima kimoja alichokipenda.
“Utulivu kabla ya dhuruba, Utulivu kabla ya dhuruba,” alirudia.
Lakini hakuogopa. Alikuwa ameweka tumaini lake lote kwa Jami na wanakijiji.



## Ziara ya rais

Hayawi, hayawi, mwisho huwa!
Ghafla, Rais alikuwa amewasili!
Jami akaruka mbele yake, mithili ya mtoto wa mbwa anavyomwongoza mmilki wake kuelekea kule apendako.
“Kila mmoja, kila mmoja, njoo ujionee!” alipiga kelele. “Ni Rais wetu!”
Rais akatabasamu huku akiwapungia mkono wanakijiji, waliomiminika kwa wingi toka katika nyumba zao. Kichwa chake chenye upara kiling’aa sawia na mng’ao wa viatu vyake katika jua la kiangazi.
Alikuwa mwenye msimamo mkali, lakini alionekana mwenye urafiki na mtulivu.
Inafurahisha, Tedi alifikiri moyoni mwake. Rais ananikumbusha upara, Teo akiwa amevalia vizuri.
Ishara nzuri! Akatabasamu wazi wazi.
Akakimbia kuungana na Teo na watoto wake wavulana, waliokuwa wakiruka juu na chini kwa shauku, kama kundi la kangaroo wa ajabu ajabu.

Punde si punde, uwanja wa mikutano ulikuwa umejaa wanakijiji wenye shauku. Rais alisimama katikati ya uwanja wa mikutano na akasubiri mpaka kila mmoja alipokuwa ameacha kupunga mikono na kuruka ruka. Akapaza asuti yake ili kijiji kizima kisikie yale aliyotaka kuyaongea.
“Rafiki yangu mpya, Jami, ameniambia mambo yote kuhusu Mtakuja na Programu ya Nishati ya Tedi,” Rais alisema. “Nimesoma repoti yenu na nimeridhishwa na ujuzi na maarifa yenu. Ni heshima kubwa kuwa hapa!” Wananchi wakapiga makofi kwa shangwe kubwa. Rais akatulia na akaangalia umati wa vichwa vya watu waliokuwa mbele yake.
“Wako wapi kina Tedi, Roza na Teo?” aliuliza.
Tedi, Roza na Teo wakatazamana wao kwa wao katika hali ya kutoamini. Rais alijuaje majina yao? “Tupo hapa mheshimiwa Rais,” hatimaye Teo alisema, akiwa anampa mkono. Akiwa amesimama pale, Tedi kwa mara nyingine akaona kufanana kati ya Rais na Teo. Hakuweza kujizuia kuzidi kumtazama Teo akiwa amevalia suti ya kifahari kama ya Rais. Akangua kicheko kwa mawazo hayo. Wanakijiji wakatazamana katika hali ya kushangaa, lakini kicheko cha Tedi kikaambukiza kijiji kizima kikaangua kicheko na hata Rais mwenyewe akaunguruma kwa kicheko.
“Samahani sana mheshimiwa Rais,” Tedi alisema. Akamshika mkono Rais. Mara nyingine huwa natengeneza taswira za kuchekesha ndani ya fahamu zangu.
“Usihofu kabisa Tedi”, Rais akajibu. “Huwa napenda kucheka!”
Kisha Rais akarudi katika hali ya utulivu tena. Akatengeza kola yake, akaweka sawa tai yake na akajiweka sawia keundelea.
“Inapendeza kukutana na watu wazuri kama nyinyi. Kwa pamoja tutaandaa mpango wa kusambaza Programu ya Nishati ya Tedi katika kila kijiji ndani ya nchi yetu! Vijiji vile vitakavyopokea Programu ya Nishati ya Tedi kwa mujibu wa taratibu mlizoanzisha hapa vitaruhusiwa kuchoma mkaa tena.”
“Oyee!” wanakijii wakashangilia kwa shauku.
Tsjirp, ndege nao waliimba.
Mei-awe, ndege tausi naye akaita.
“Bzzz,” nyuki nao wakadakia, mpaka kijiji kilipojazwa na mamilioni ya sauti za furaha.



## Programu ya Nishati ya Tedi

Asubuhi iliyofuata, wanakijiji wote walikutana na Rais katika uwanja wa mikutano. Kwa pamoja wakaongea kuhusu njia nzuri ya kuweza kusambaza Programu ya Nishati ya Tedi katika vijiji vingine nchini. Mwisho wa siku ile walikuwa wameshaandaa mpango kazi.
“Kesho, tutazindua Programu ya Nishati ya Tedi kitaifa!” Rais alisema.
“Nitaomba nyinyi nyote mnisaidie.”
“Hatutakuangusha!” wanakijiji wakajibu kwa shangwe.
Hivyo Nishati ya Tedi ikawa ndiyo chapa ya taifa ya mkaa endelevu, iliyopendwa na watu na wanyama wote duniani. Wakati wa maadhimisho ya sabini ya siku ya kuzaliwa ya Tedi, Teo akambusu mkewe kichwani, Rashidi na Joni wakampiga-piga mabutu ya nywele zake na wajukuu zake wawili wakamkumbatia miguu yake. Mama yao, Maria, alitabasamu kwa furaha katika tukio hilo. Tedi aliangalia uwanda wa kijiji uliopendeza kwa rangi nzuri za kuvutia. Hewa ilikuwa imejaa harufu ya mvua baada ya kiangazi kirefu.
“Ndugu wanakijiji,” Tedi alisema.
“Najivunia kusema kuwa vijiji vyote katika nchi yetu sasa vinachoma mkaa kwa kutumia chapa ya Nishati ya Tedi!”
Kishindo cha nderemo na kelele za shangwe vikasikika.
“Oyee! Maisha marefu Tedi!”
Tedi alitabasamu wazi wazi. Uso wake wote ukabadilika kuwa kama mguu wa kunguru mwenye furaha. Mara macho yake yakarudi katika utulivu. Akasimama juu na kuinua mkono wake.
“Hakuna lolote la ajabu kuhusu mimi,” Tedi alisema. “Kama ambavyo hakuna lolote la ajabu juu ya mtu yoyote duniani. Ilikuwa ni mchanganyiko wa bidii ya kazi, uvumilivu, upendo na bahati kiasi ndivyo vimetufikisha hapa tulipo. Programu ya Nishati ya Tedi ingeweza kuwa Programu ya Nishati ya Mohamedi, ya Azizi, ya Roza!”
Wanakijiji wakatikisa vichwa. Maneno ya Tedi yakawajaza kiburi.
“Nishati ya Tedi ni nishati zetu wote zikichanganywa pamoja!” Tedi alisema
“Msisahau jambo hili!”
“Tunaweza tukawa tumetatua tatizo hili lakini mara zote kutatokea matatizo mengine ya kutatua siku zijazo. Kwa pamoja, kila mmoja wenu anaweza kuongoza mchakato wa kutatua matatizo hayo ilimradi tunafanya kazi kwa mshikamano.”
Ghafla, jitu kubwa likaingia katika uwanja wa mikutano. Wanakijiji walilishangaa jitu hilo lilipopenya katikati ya umati wa watu. Tedi hakuamini macho yake.
“TUUT!”

Mkonga wenye makunyanzi ukambeba Tedi na kumzungusha hewani.
“TEMBO!” Tedi akashangilia hatimaye.
Tedi akakumbatia mkonga wa Tembo kwa nguvu. Tembo akafumba macho yake yaliyo mithili ya zabibu.
“Tuutuut”
“Najua hiyo ‘Tuuttuut’ Tembo, Tedi alisema. “Inamaanisha, ninakusikia. Sasa hebu ondoka, unanibana pumzi ewe msichana mwenye wazimu, au siyo?”
Tembo alifumba macho. Tedi alicheka.
“Nimefurahi sana kukuona wewe rafiki yangu!” akasema. “Hebu twende kwenye ziara ya msituni”.Kwa pamoja, Tembo na Tedi wakatembea kuingia msituni wakiangalia vipepeo, ndege tausi na matunda yenye juisi.



## Kuhusu kitabu hiki


Nishati ya Tedi ni kitabu kwa ajili ya watoto kati ya miaka 10 hadi 14. Kimeandikwa kwa malengo mawili: (i) kuelimisha watoto wa Tanzania na watoto katika dunia yote kuhusu uchomaji wa mkaa endelevu, na (ii) kukusanya ufandhili kwa ajili ya kuwasilisha matokeo ya utafiti wangu wa Shahada ya Uzamivu (PhD) kwa vijiji sita vya Tanzania ambako kazi ya ukusanyaji takwimu za utafiti ilifanyika. Tumaini langu ni kuwa katibu cha Nishati ya Tedi kitawawezesha watoto kote ulimwenguni na kuwafanya watambue kuwa kila mmoja ana uwezo na jukumu la kulinda mazingira asilia na kuyarejesha pale inapogundulika kuwa yameharibiwa.

*Kuhusu Mradi wa Jamii Zilizoshiriki Katika Utafiti*
Wazo la kuandika kitabu cha Nishati ya Tedi liliibuka mwishoni mwa masomo yangu ya Shahada ya Uzamivu katika Kitengo cha Sayansi ya Mfumo wa Dunia cha Chuo Kikuu cha Zurich nchini Uswisi. Wakati wa masomo yangu, nilifanya utafiti kuhusu uchomaji wa mkaa ili kupata ufahamu wa kina juu ya matokeo ya mifumo ya usimamizi wa misitu katika uchomaji wa mkaa na maisha ya wachoma mkaa. Utafiti huu unaweza kutumika kufahamisha na kuboresha zaidi mifumo iliyopo ya usimamizi wa misitu kwa ajili ya uchomaji wa mkaa. Sehemu kubwa ya utafiti huu ilijikita katika mahojiano na wachoma mkaa na wataalamu kuhusu riziki na uchunguzi wa ndani wa hali ya misitu ya asili katika vijiji sita vya wilaya ya Kilosa, Tanzania.

Kwa sasa, bado ni kawaida kwa watafiti toka ulimwengu wa Kaskazini kufanya tafiti katika maeneo ya ulimwengu wa Kusini bila kushirikisha watu kikamilifu, na/au kutoa mrejesho wa matokeo ya utafiti. Dhana hii inaitwa “utafiti wa helikopita” na dhana hii haitoi faida kabisa au inatoa faida chache sana kwa nchi na jamii zile zinazohusishwa katika utafiti. Ili jamii ziweze kufaidika kutokana na matokeo ya utafiti wa kisayansi, ni jambo la muhimu sana kuhakikisha matokeo ya utafiti yanawafikia wanajamii moja kwa moja. Kwa upande wetu, vijiji sita na Wilaya ya Kilosa wanaweza kutumia matokeo ya utafiti wetu kuchangia katika kuboresha usimamizi wa misitu au katika kufanya utetezi kuhusu mabadiliko ya sera husika.

Ili kuwasilisha matokeo ya utafiti wa Shahada yangu ya Uzamivu kwa vijiji sita husika na wilaya ya Kilosa, ni muhimu mimi kuweza kufika huko ana kwa ana. Hii inahitajika kwa sababu hakuna mtandao wa intaneti katika vijiji hivyo na pia kwa kuwa ni desturi katika Tanzania kujadili na kupeana taarifa kwa njia ya kuonana ana kwa ana. Pamoja na watafiti wawili wa Tanzania, ambao nilishirikiana nao kwa karibu wakati wa masomo yangu ya PhD, ninalenga kusafiri kwenda katika vijiji hivyo sita na wilaya ya Kilosa mnamo mwezi Februari 2024 ili kuwasilisha kwao matokeo ya utafiti wetu. Tunalenga kuwasilisha matokeo hayo katika mfumo wa warsha, mabango na kitabu hiki cha Nishati ya Tedi. Lengo ni kutoa taarifa kwa jamii husika na kuamsha mjadala miongoni mwa wanavijiji ili kuwezesha kuboresha mifumo ya usimamizi wa misitu yao kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu. Tunatumaini kuwa hii itawezesha wao kuweza kubaini baadhi ya mambo wanayohitajika kufanya ili kulinda mazingira na kuweza kupata faida kutokana na kuchoma mkaa.

*Marejeleo*
1. Haelewaters, D., Hofmann, T.A., Romero-Olivares, A.L. 2021. “Ten simple rules for Global North researchers to stop perpetuating helicopter research in the Global South.” PLoS Comput Biol 17(8): e1009277. https://doi.org/10.1371/journal.pcbi.1009277



Nishati ya Tedi ni kitabu cha hadithi za kisasa kuhusu mambo ya zamani kuhusu wanadamu.

Siku moja, Tedi anakutana na mgeni wa ajabu katika msitu wa kijiji chake kizuri, Mtakuja. Mgeni anageuka kuwa mfanyabiashara wa mkaa ambaye aliwashawishi wanakijiji wote kumchomea mkaa kutoka katika msitu wao. Tedi alifurahia sana tukio hilo. Kutokana na kuchoma mkaa, hitamaye wazazi wake walipata pesa na kuweza kumudu kumsomesha Tedi! Anaporudi kijijini kwao baada ya kusoma kwa miaka mingi, anakuta kijiji kimegeuka jangwa mahali ambapo awali kulikuwa na msitu mzuri. Takribani miti yote imetumika kuchoma mkaa. Baada ya msitu wote kutoweka maisha ya wanakijiji yapo hatarini. Tedi amechanganyikiwa. Pamoja na wanakijiji wenzake na marafiki anafanya mpango wa kurejesha upya msitu na kukiondoa kijiji chao kutoka katika umaskini. Je, watapata namna ya kusimamia ardhi na msitu wao kwa njia endelevu?